`

TANZANIA HIGHER LEARNING INSTITUTIONS TRADE UNION
(THTU)

(CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA)

KATIBA YA CHAMA

TOLEO LA MWAKA 2016

YALIYOMO

DIBAJI....3
FASILI....4
SEHEMU YA KWANZA....5
1.0 UTANGULIZI....5
1.1 TAFSIRI YA MANENO YATUMIKAYO KATIKA KATIBA....5
1.2 JINA NA IMANI YA CHAMA....7
1.3 MAKAO MAKUU YA CHAMA NA ANUANI....7
1.4 USHIRIKIANO....7
1.5 IMANI YA CHAMA....7
1.6 USHIRIKIANO NA VYAMA VYA SIASA....8
SEHEMU YA PILI....8
2.0 MADHUMUNI....8
SEHEMU YA TATU....9
3.0 UANACHAMA....9
3.1 MAOMBI YA UANACHAMA....9
3.2 AINA ZA WANACHAMA....10
3.3 MICHANGO YA MWANACHAMA....10
3.4 KADI ZA UANACHAMA NA DAFTARI LA KUMBUKUMBU....11
SEHEMU YA NNE....11
4. 0 HAKI ZA MWANACHAMA....11
4.1 WAJIBU WA MWANACHAMA....11
4. 2 KUSIMAMISHWA AU KUACHISHWA UANACHAMA....12
4.3 KUHAMA SEHEMU YA KAZI AU SEKTA YA KAZI....13
4.4 UTARATIBU WA KUJIUZULU UANACHAMA....13
SEHEMU YA TANO....13
5.0 MUUNDO WA CHAMA, UONGOZI, VIKAO VYA MAAMUZI NA KAMATI ZA UTENDAJI....13
5.1 MUUNDO WA CHAMA....13
5. 2 MUUNDO WA UONGOZI NGAZI YA TAIFA....14
5.3 MUUNDO WA UONGOZI NGAZI YA TAWI....19
5.4 VYOMBO VYA MAAMUZI VYA CHAMA....21
5.5 KAMATI ZA UTENDAJI ZA CHAMA....27
SEHEMU YA SITA....33
6.0 TARATIBU ZA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA CHAMA....33
6.1 MKUTANO MKUU WA UCHAGUZI WA TAWI....33
6.2 UCHAGUZI NGAZI YA TAIFA....35
SEHEMU YA SABA....36
7.0 KAMATI MBALIMBALI ZA CHAMA....36
7.1 KAMATI YA MAADILI NA UTAWALA BORA YA CHAMA....36
7.2 KAMATI ZA USHAURI YA CHAMA....36
SEHEMU YA NANE....37
8.0 MAPATO YA CHAMA....37
8.1 UPATIKANAJI WA FEDHA....37
8.2 KANUNI ZA MATUMIZI YA FEDHA....37
8.3 UKAGUZI WA FEDHA NA MALI ZA CHAMA....37
SEHEMU YA TISA....38

9.0. UTUMISHI KATIKA CHAMA 38
SEHEMU YA KUMI 38
10. MENGINEYO 38
10.1 KIWANGO CHA MAHUDHURIO YA MIKUTANO 38
10.2 NAFASI KUWA WAZI 38
10.3 KUJAZA NAFASI ZILIZO WAZI 39
10.4 KUJIUZULU UONGOZI 39
10.5 KUJITOLEA KWA AJILI YA CHAMA 39
10.6 KUSIMAMISHWA UONGOZI 39
10.7 KUACHISHWA/KUSIMAMISHWA UONGOZI 39
10.8 MAHUDHURIO YA MIKUTANO 40
10.9 TARATIBU ZA UCHAGUZI 40
10.10 KUJIDHIHIRISHA KWA VIONGOZI 40
10.11 KURA YA KUTOKUWA NA IMANI 40
10.12 KANUNI MBALIMBALI ZA CHAMA 40
SEHEMU YA KUMI NA MOJA 41
11.0. TAFSIRI 41
SEHEMU YA KUMI NA MBILI 41
12.0. KUVUNJIKA KWA CHAMA AU KUUNGANISHA VYAMA 41
12.1 KUVUNJIKA CHAMA 41
12.2 KUUNGANISHA VYAMA 41
SEHEMU YA KUMI NA TATU 41
13.0. MIGOGORO YA KIKAZI, MIJADALA NA MWENENDO 41
13.1 SERA YA UJUMLA 41

DIBAJI

Katiba hii ni ya Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU) na ndiyo iliyowezesha Chama kusajiliwa tarehe 12/12/2008 na kupewa hati ya usajili namba 23.

Mabadiliko ya Katiba ya sasa yanatokana na maoni ya marekebisho kutoka kwa wanachama matawini kwa kuzingatia Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini No 6 ya mwaka 2004, mabadiliko ya Soko la Kazi pamoja na Miundo ya Utumishi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania na, zaidi sana, kujaribu kuleta ufanisi na tija katika kuwahudumia wanachama wote na taifa kwa ujumla. Mabadiliko haya yalifuata tararibu zote za utawala bora kwa kufuata mchakato wa vikao mbalimbali vya chama hadi kufika ngazi ya mwisho ya maamuzi yani Mkutano mkuu kwa mujibu wa katiba hii.

THTU inamilikiwa na kuendeshwa kwa misingi ya ushiriki wa wanachama wake kupitia vyombo vyake vya uwakilishi vya ngazi za tawi na taifa. Mambo ya msingi ambayo THTU inazingatia ni kuimarisha mshikamano, umoja na usawa miongoni mwa wanachama wake na wanachama wengine wa vyama vya wafanyakazi vya ndani na nje. Aidha, Chama kinaendelea kuimarisha mahusiano mazuri baina yake na Mabaraza ya Wafanyakazi, Vyama vya Kitaaluma, Waajiri, Serikali na Wadau wengine wote bila kuathiri uhuru wake. Chama kitaendelea kusimamia utetezi imara wa haki na maslahi ya wafanyakazi, ajira na usawa, hadhi na masuala yote yahusuyo Hifadhi na Ustawi wa Wafanyakazi ndani na nje ya Taasisi zake.

Katiba hii ya THTU ya mwaka 2016 ndio itakayoongoza utekelezaji wa shughuli/kazi za Chama katika ngazi zote. Aidha, Katiba hii itaendelea kufanyiwa marekebisho kadiri wanachama, kupitia halmashauri zao watakavyoona inafaa na kwa kuzingatia kanuni za Katiba hii na Sheria za nchi. Wanachama, viongozi, maafisa na watendaji wote wa Chama katika ngazi zote hawana budi kuheshimu katiba hii pamoja na Sheria za Nchi.

.....
Yusuph Singo Omari
MWENYEKITI THTU TAIFA

FASILI

Mahala popote ambapo maneno yanatamkwa, hapa chini katika Katiba hii, yametumika kwa maana au ufafanuzi au fasili iliyotolewa kisheria iwapo pana sheria yoyote nchini kuhusiana nayo, vinginevyo kwa maana inayokubalika na Chama.

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Katiba hii itarejewa na kujulikana kama **Katiba ya Chama Cha Wafanyakazi wa Elimu ya Juu Tanzania, 2016.**

Katiba hii haitaaathiri kwa namna yoyote ile sheria za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na iwapo utatokea mgogoro wowote katika tafsiri ya Katiba hii basi sheria za nchi zitatumika kutatua mgogoro huo.

Ili kuondoa utata katika tafsiri na maana ya katiba hii, popote ambapo maneno yafuatayo yatajitokeza, yatatafsiriwa kulingana na kipengele hiki cha maana ya maneno yaliyotumika katika Katiba hii.

1.1 TAFSIRI YA MANENO YATUMIKAYO KATIKA KATIBA

"Chama" – Ina maana ya Chama cha Wafanyakazi wa Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania.

"THTU" – Ina maana ya ufupisho wa jina la Chama kwa Kiingereza.

"Mkutano Mkuu" – Ina maana ya Mkutano Mkuu wa Chama ki-Taifa au Chombo/Kikao cha juu kabisa cha maamuzi katika Chama au kama inavyofafanuliwa na Katiba hii.

"Baraza Kuu" – Chombo cha pili kwa madaraka ya maamuzi katika Chama au kama inavyofafanuliwa na Katiba hii.

"Kamati ya Utendaji" - Chombo cha tatu chenye mamlaka ya kiutendaji katika Chama au kama inavyofafanuliwa katika Katiba hii.

"Kamati ya Maadili" – Chombo huru katika muundo wa chama cha kusimamia maadili ya viongozi na wanachama ili kujenga misingi ya uadilifu, utawala bora na taswira chanya

"Tawi" – Ina maana eneo la uongozi wa chama ambalo ndilo msingi wa chama na chimbuko la wanachama, ambao ndio chama chenyewe kwa mujibu wa Katiba hii.

"Kamati ya Ushauri" – Chombo cha kumshauri Mwenyekiti wa chama taifa katika masuala ya dharura na mengine nyeti pale itakapobidi

"Mkutano Mkuu wa Tawi" – Chombo chenye maamuzi ya mwisho katika Chama kwenye Tawi kama inavyofafanuliwa na Katiba hii.

Katibu Mkuu – Mratibu Mkuu wa Chama au kama inavyofafanuliwa na Katiba hii.

"Mweka Hazina"– Mshauri Mkuu wa Vikao vya Kikatiba vya Chama Kitaifa juu ya masuala au taratibu za Fedha na rasilimali za Chama.

"Mkuu wa Idara" – Ina maana ya Mtumishi na Mratibu Mkuu katika Idara ya Chama kama inavyofafanuliwa na Katiba hii.

"Katibu wa Tawi" – Ina maana ya Mtendaji wa Chama katika Tawi au kama inavyofafanuliwa na Katiba hii.

"Kiongozi" – Ina maana ya mwanachama yeyote katika Chama ambaye madaraka au mamlaka au nafasi yake katika shughuli za Chama ameipata kupitia uchaguzi au kama inavyofafanuliwa na Katiba hii.

"Afisa wa Chama" - Mwanachama yeyote aliyeteuliwa na kikao au mamlaka mbalimbali za chama kufanya kazi za chama.

“Mtumishi Mtendaji” – Ina maana ya mtu yeyote katika Chama ambaye utendaji wa kazi, madaraka, mamlaka au nafasi yake katika shughuli za Chama ameipata kupitia fursa ya ajira katika Chama au kama inavyofafanuliwa na Katiba hii.

“Mtumishi” – Ina maana ya mtu yeyote kwenye Chama, ambaye madaraka, mamlaka au nafasi aliyonayo katika shughuli za Chama ameipata kupitia fursa ya ajira.

“Mwajiri”– Ina maana mtu binafsi, kampuni, shirika, taasisi ama serikari ambaye ameingia makubaliano/mkataba wa kazi na mtu ama watu fulani kwa madhumuni ya kumfanyia kazi na yeye kulipa ajira.

“Mfanyakazi” – Ina maana ya mwajiriwa au mtu yeyote aliyeingia katika Mkataba/Makubaliano na mwajiri ya kutumia taaluma kama nyezo na nguvu kazi yake kuzalisha mali au kutoa huduma kwa malipo yanayothaminika kifedha kwa kila saa ya uzalishaji mali au huduma.

“Mwanachama” – Ina maana ya Mfanyakazi yeyote aliye katika ajira ya Taasisi ya Elimu ya Juu ambaye amekubali kujiunga na Chama na kukidhi matakwa ya kisheria na katiba ya chama.

“Mwanachama hai” – Ina maana ya mwanachama anayeshiriki, kwa ukamilifu, katika shughuli mbalimbali za chama na kufahamu malengo na mwelekeo wa chama, hii ikiwa ni pamoja na kushiriki katika vikao na mikutano ya chama pamoja na kutoa michango kwa mujibu wa taratibu za chama.

“Makubaliano au Mkataba” – Ina maana ya maelewano yaliyofikiwa kati ya mwajiri na Mfanyakazi au Chama chake kwa niaba ya mwanachama/wanachama.

“Mgogoro” – Ina maana ya kuwepo kwa matatizo yanayotokana na mazingira ya kikazi au kuwepo kwa hali isiyokuwa ya maelewano kati ya Mwajiri na Mfanyakazi/Wafanyakazi/Chama kuhusiana na ajira au maslahi yanayoambatana nayo.

“Mgomo” – Ina maana ya kusimama kwa shughuli zinazoendeshwa na Mwajiri kutokana na kutotendwa na wafanyakazi kwa shughuli hizo kwa sababu ya kutokuwepo kwa maelewano kati yao (Mwajiri na Wafanyakazi) kuhusiana na suala au masuala ya ki-ajira.

“Shirikisho” – muungano wa vyama huru vya wafanyakazi.

“Serikali” – Ina maana ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Chombo chenye madaraka ya utawala kwa eneo au nchi ambayo Chama hiki kinaendesha shughuli zake.

“Msajili” – Ina maana ya Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi nchini au kama inavyofafanuliwa na sheria za Vyama vya Wafanyakazi.

“Kamishna wa Kazi” – Ina maana ya Mwakilishi wa Serikali juu ya masuala yahusuyo Sheria au Kanuni au taratibu za Ajira/Kazi nchini.

“Afisa wa Kazi” – Ina maana ya Mwakilishi wa Serikali juu ya masuala yahusuyo Sheria au Kanuni au taratibu za Ajira/Kazi nchini.

“Makato ya uwanachma” – Ina maana ya utaratibu wa kupata, kwa hiari, michango ya mwanachama kwa Chama chake anayolipa kwa kukatwa moja kwa moja na mwajiri kutokana na mshahara wake au kama inavyofafanuliwa na Sheria za nchi..

“Mwenyekiti” – Ina maana msemaji mkuu wa chama katika ngazi husika ya chama.

“Kamati ya Wanawake ” – Ina maana kamati inayojumuisha wanawake wanachama katika ngazi mbalimbali ya chama kwa ajili ya kutafutia ufumbuzi matatizo ya wafanyakazi wanawake katika ajira na jamii inayotuzunguka.

"Taasisi za Elimu ya Juu"- Taasisi zote zinazohusika na utoaji na usimamizi wa elimu ya juu

1.2 JINA NA IMANI YA CHAMA

1.2.1 Chama, kwa lugha ya Kiingereza, kitaitwa **TANZANIA HIGHER LEARNING INSTITUTIONS TRADE UNION.**

1.2.2 Chama, kwa lugha ya Kiswahili, kitajulikana kama **CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA**

1.2.3 Kifupisho cha Jina la Chama kwa lugha ya Kiingereza kitakuwa kinasomeka **THTU** na ndicho kifupisho halisi kitakachotumiwa na chama katika mawasiliano yake

1.3 MAKAO MAKUU YA CHAMA NA ANUANI

Makao Makuu ya Chama yatakuwa **Dar es Salaam** na Anuani yake itakuwa **S.L.P. 35928, DAR ES SALAAM**, Tanzania. Simu: 022 2401581 Nukushi: 022 2401582
Tovuti: www.thtu.or.tz Barua pepe: katibu@thtu.or.tz au info@thtu.or.tz

1.4 USHIRIKIANO

1.4.1 Kujishirikisha Hapa Nchini

Chama kitakuwa huru kujishirikisha na Shirikisho lolote la Vyama vya Wafanyakazi lililopo nchini au kushirikiana na vyama vingine kuunda Shirikisho.

Aidha, Wakati wa kujiunga, chama kitapata ridhaa kutoka kwa angalau nusu ya wajumbe wa Mkutano Mkuu. Chama kitakuwa kinatoa taarifa ya namna kinavyojishirikisha katika Mkutano Mkuu wa chama

1.4.2 Kujishirikisha Kimataifa

Chama kitakuwa huru kujishirikisha na vyama vingine vya wafanyakazi duniani kwa madhumuni ya kubadilishana ujuzi, uzoefu na takwimu za kitafiti kuhusu sekta zilizo na wanachama.

1.5 IMANI YA CHAMA

Chama kinaamini kuwa:

i) Wafanyakazi wote ni sawa na ni injini na uti wa mgongo wa maendeleo na uchumi wa taifa lolote;
ii) Kila mfanyakazi ana haki ya kufanya kazi na kupata ujira linganifu;
iii) Kila mfanyakazi anastahili haki ya kufanya kazi katika mazingira yasiyotweza;
iv) Mshikamano wa wafanyakazi wote duniani ndiyo njia pekee itakayokuza ushirikiano wa karibu kati ya wafanyakazi na vyama vyao katika nchi zote;
v) Utengano wa aina yoyote kati ya wafanyakazi ni alama ya udhaifu;
vi) Kila mfanyakazi anastahili malipo ya haki ya hifadhi ya maisha yake wakati wa uzee kutoka katika mifuko ya hifadhi ya jamii;
vii) Kwamba wafanyakazi watatumia majadiliano kama nyenzo muhimu katika mchakato wa kuboresha maslahi na ustawi wa ajira zao na mazingira kazi yanayowazunguka;
viii) Kwamba umoja huo ndio chachu ya maendeleo ya Taifa na ukombozi wao;
ix) Kwamba nguvu kazi iliyoelimika na kuwezeshwa, ni kinga thabiti kwa majanga yatokanayo na mazingira kazi;
x) Kila mfanyakazi atakuwa huru kujiunga na chama chochote cha siasa atakachopendelea;

1.6 USHIRIKIANO NA VYAMA VYA SIASA

THTU ni chama ambacho hakitashirikiana na chama chochote cha siasa nchini katika shughuli za kisiasa.

SEHEMU YA PILI

2. MADHUMUNI

Madhumuni makuu ya chama yatakuwa ni haya yafuatayo:

2.1 Kusimamia na kutetea haki na maslahi ya wafanyakazi;

2.2 Kushirikiana na kujadiliana na waajiri katika kudumisha amani kwa kuboresha mazingira na maslahi ya wafanyakazi mahala pa kazi;

2. 3 Kuhakikisha kwamba mwajiri anafuata na kuziheshimu sheria za kazi;

2. 4 Kulinda, kuheshimu na kutekeleza makubaliano ya pamoja yaliyojadiliwa na kukubaliwa kati ya Chama na Mwajiri;

2. 5 Kutekeleza na kusaidia katika utekelezaji wa mikataba ya hali bora za kazi, tuzo na kanuni za nidhamu kulingana na sheria za kazi;

2. 6 Kushirikiana na kubadilishana ujuzi na vyama vingine vya wafanyakazi nchini pamoja na vile vya kimataifa kwa madhumuni ya:

i. Kupata, kutunza na kutoa taarifa au elimu katika masuala muhimu yahusuyo vyama vya wafanyakazi;
ii. Kubadilishana ujuzi na taarifa katika masuala yanayohusiana na mishahara, hali za wafanyakazi na taratibu za kimataifa zinazohusiana na masuala hayo;
iii. Kufikisha, kwa wafanyakazi kote nchini, taarifa zozote muhimu zihusuzo kazi, mazingira ya kazi na maslahi yao, zitokanazo na Elimu na tafiti mbalimbali.

2. 7 Kujadiliana na Serikali kuhusu utungwaji wa sheria zinazohusu haki na stahili za kazi na kuandaa sera nzuri za kuendeleza uchumi na maisha ya jamii kwa ujumla;

2. 8 Kuwaunganisha wafanyakazi na kutumia umoja wao kama nyenzo muhimu ya kujikwamua na mazingira kazi duni;

2.9 Kuwa kitovu cha utafiti na ukusanyaji wa takwimu, kuhusu hali na mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi na kutumia tafiti na takwimu hizo kuishauri serikali kuboresha maisha ya wafanyakazi.

SEHEMU YA TATU

3. UANACHAMA

3.1 MAOMBI YA UANACHAMA

Wafanyakazi wote wa Taasisi za Elimu ya Juu nchini watakuwa na hiari ya kuwa wanachama wa **THTU** kwa mujibu wa katiba hii. :

Masharti ya kuwa mwanachama ni haya yafuatayo:-

i. Mwanachama wa **THTU** sharti awe mfanyakazi wa Taasisi ya Elimu ya Juu, Chuo cha Elimu ya Juu au Taasisi ya Usimamizi wa Elmu ya Juu na awe ni raia wa Tanzania;
ii. Ajaze fomu maalum ya kujiunga na chama cha wafanyakazi kwa mujibu wa sheria.
iii. Maombi ya wanachama wapya yatapelekwa kwenye ofisi ya tawi mahala pa kazi anapofanyia kazi muombaji;
iv. Uongozi wa tawi, bila kuchelewa, utachambua, kufikiria na kuyakubali maombi hayo. Uongozi wa tawi ukiyakataa maombi, utawajibika kutoa sababu za uamuzi huo kwa halmashauri ya tawi.
v. Tawi litawasilisha Fomu/Taarifa hizo Makao Makuu ya Chama.

3.2 AINA ZA WANACHAMA

Kutakuwa na aina mbili za wanachama:

3.2.1. Wanachama wa Kawaida – hawa ni wanachama ambao wangali kazini na hawajafikia umri wa kustaafu kisheria.

3.2.2. Wanachama Walio kwenye Ajira za Mkataba wa muda maalum– hawa ni wanachama wanaofanya kazi katika Taasisi za Elimu ya Juu, Vyuo vya Elimu ya Juu au Taasisi za Usimamizi wa Elimu ya Juu na wenye Ajira za Mikataba.

3.3 MICHANGO YA MWANACHAMA

3.3.1 Kiingilio

Hakutakuwa na kiingilio cha mtu anayejiunga na chama. Mtu akishajaza fomu ya kujiunga na chama, tayari amesharidhia kukatwa sehemu ya mshahara wake kuchangia chama kama inavyoelezwa.

3.3.2 Michango ya kila Mwezi

i. Mwanachama atalipa ada ya asilimia moja kutoka katika mshahara wake kila mwezi na endapo asilimia moja ya mshahara wa mwanachama itazidi kiasi za shilingi elfu ishirini mwanachana atalipa elfu ishirini tu.
ii. Michango ya wanachama itapelekwa kwenye Makao Makuu ya Chama ikiambatanishwa na orodha ya wanachama waliochangia ili kurahisisha ukaguzi wa hesabu za chama;
iii. Malipo yote yatakayofanywa na mwanachama, yatapelekwa benki katika akaunti iliyofunguliwa na Chama - Makao Makuu;
iv. Chama - Makao Makuu, kitapeleka asilimia hamsini ya ada za wanachama kwenye akaunti iliyofunguliwa na tawi na asilimia hamsini itabaki kwenye akaunti ya Makao Makuu.
v. Endapo kutatokea mabadiliko yeyote katika viwango vya ada maamuzi juu ya mabadiliko hayo yatafanywa na Mkutano kuu kwa mujibu wa katiba hii.

3.3.3 Michango Maalumu

Kila watakapotakiwa, wanachama watawajibika kutoa michango maalumu kwa kadiri itakavyoamuliwa na vikao vya chama katika masuala yanayohusiana na migogoro au masuala mengine mahali pa kazi kwa maslahi ya wanachama.

Aidha, michango yote ya ziada lazima iridhiwe na kamati ya Utendaji ya Chama.

3.4 KADI ZA UANACHAMA NA DAFTARI LA KUMBUKUMBU

3.4.1 Kadi ya Uanachama

Kila mwanachama atapewa kadi iliyochapishwa ambayo ndani yake itajazwa jina lake, tawi anapotoka, namba ya uanachama kutoka kwenye tawi lake, sahihi ya mwanachama, sahihi ya Katibu Mkuu wa chama na maelezo mengine yoyote kama yalivyoelekezwa na kanuni au taratibu za chama.

3.4.2 Daftari la Kumbukumbu

Maelezo yote ya mwanachama yaliyomo katika kadi ya uanachama yataingizwa katika daftari la kumbukumbu za uanachama kwa madhumuni ya kusaidia kuhifadhi kumbukumbu.
Chama kitatunza Orodha ya majina ya wanachama wake kwa mujibu wa sheria.

SEHEMU YA NNE

4. 0 HAKI ZA MWANACHAMA

Mwanachama atakuwa na haki zifuatazo:

i. Kuwakilishwa na Chama dhidi ya masuala ya nidhamu mbele ya mwajiri wake na kujitetea yeye mwenyewe dhidi ya mwajiri huyo kwa mashitaka dhidi yake;
ii. Mwanachama au tawi atakuwa/litakuwa na haki ya kupeleka hoja zake katika vikao vya ngazi mbalimbali za chama; aidha hoja hizo lazima zimfikia Katibu wa Tawi kabla ya kuzipelekwa na kujadiliwa
iii. Kujitetea mbele ya vyombo mbalimbali vya chama na haki ya kuomba rufaa katika vyombo vya juu vya chama pale ambapo hataridhika na uamuzi uliotolewa;
iv. Kila mwanachama atakuwa na haki ya kuchaguliwa au kuchagua kiongozi kwa kufuata taratibu za katiba na kanuni za chama bila kuzikiuka, Kushiriki katika shughuli zote za chama na mikutano kwa mujibu wa Katiba hii;
v. Kupata taarifa za hesabu za fedha za chama kadri zitakavyohitajika
vi. Kupata taarifa na mrejesho wa vikao mbalimbali vya chama.

4.1 WAJIBU WA MWANACHAMA

Kila mwanachama atakuwa na wajibu wa:

i. Kushirikiana vilivyo na Chama katika kuwezesha mazingira bora ya kazi mahala pa kazi;

ii. Kulipa michango ya kila mwezi;
iii. Kuunga mkono na kushiriki vilivyo katika masuala ya uendeshaji wa shughuli za Chama;
iv. Kufahamu, kuzingatia na kulinda Katiba ya Chama;
v. Kuhudhuria vikao vyote vya Chama vinavyomhusu;
vi. Kuheshimu maamuzi yaliyofanywa na Chama kwa mujibu wa katiba;
vii. Kutoa michango maalum pindi anapoombwa kufanya hivyo.

Aidha, Mwanachama ambaye hatalipa michango yake kwa miezi mitatu mfululizo bila sababu za msingi zinazokubaliwa na Halmashauri ya Tawi atakuwa amejiachisha uanachama.

4. 2 KUSIMAMISHWA AU KUACHISHWA UANACHAMA

4.2.1 Sababu za Kusimamishwa au Kuachishwa:

Mwanachama yoyote anaweza kusimamishwa au kuachishwa uanachama kama atafanya yafuatayo:

i. Atagundulika kuwa alijipatia uanachama bila kufuata taratibu za kujiunga na Chama kama zilivyoainishwa katika Sheria za Kazi ;
ii. Kwa kukosa uaminifu, amefuja au kupoteza mali ya chama;
iii. Atagundulika kuwa ni mwananchama wa Chama kingine cha Wafanyakazi;
iv. Atafanya vitendo vinavyopingana na Katiba ya Chama;
v. Ametumia jina na nembo ya chama bila idhini ya Katibu wa Chama
vi. Ametoa siri za Chama kwa watu wasiohusika na ama kufanya shughuli zinazofanywa na Chama
vii. Ameanzisha mapinduzi ya kiuongozi na kiitikadi dhidi ya Viongozi na Wanachama kwa ujumla
viii. Amekisaliti Chama katika masuala ya migogoro ya kikazi.

4.2. 2 Utaratibu wa Kusimamishwa au Kuachishwa Uanachama:

i. Endapo Mwanachama ataonekana ana dosari inayoweza kuleta mtikisiko katika Chama, atapewa muda wa mwezi moja kujitetea kabla ya hatua nyingine kuchukuliwa;
ii. Halmashauri ya Tawi itatoa mapendekezo ya kumfukuza Mwanachama na kutoa taarifa za shauri hilo kwa Kamati ya Utendaji ya Taifa baada ya muda wa kurekebisha dosari kumalizika.
iii. Kamati ya Utendaji ya Taifa itayapitia mapendekezo ya Kamati ya Tawi ndani ya siku saba na kuliwasilisha suala hilo kwa Kamati ya Maadili ya Chama.
iv. Kamati ya Maadili italijadili suala husika ndani ya siku kumi na nne (14) na kupeleka mapendeko yake kwenye Mkutano wa Baraza Kuu.
v. Mwanachama, kabla ya kusimamishwa/kuachishwa, atapewa fursa ya kusikilizwa na kujitetea katika ngazi zote husika, na endapo hataridhika na

maamuzi ya Kamati ya Maadili atakata rufaa kwenye Baraza kuu la chama.

4.3 KUHAMA SEHEMU YA KAZI AU SEKTA YA KAZI

4.3.1 Kuhama kwa Mwanachama kutoka sehemu moja ya kazi kwenda sehemu nyingine ya Sekta ya Chama, hakutaondoa Uanachama wake;

4.3.2 Mwanachama atakayehama kutoka kwenye sekta moja ya chama kwenda sekta nyingine ana hiari ya kubaki na Uanachama na Tawi lake mama au kuhamishia Uanachama wake kwenye Tawi jipya;

4.3.3 Mwanachama akatayependa kujiunga na Chama toka Chama kingine shiriki katika shirikisho atawajibika kuomba upya uanachama.

4.4 UTARATIBU WA KUJIUZULU UANACHAMA

4.4.1. Mwanachama ana uhuru wa kujiuzulu uanachama wake wakati wowote kwa kumwandikia katibu wa Tawi lake taarifa ya mwezi mmoja;

4.4.2 Mwanachama ambaye uanachama wake utakoma katika Chama, kwa mujibu wa Katiba hii, atapoteza haki za uanachama;

4.4.3 Mwanachama atakayepoteza uanachama, hatarudishiwa michango yake aliyokuwa anakatwa wakati wa uanachama wake

SEHEMU YA TANO

5.0 MUUNDO WA CHAMA, UONGOZI, VIKAO VYA MAAMUZI NA KAMATI ZA UTENDAJI

5.1 MUUNDO WA CHAMA

Muundo wa Chama utakuwa na ngazi mbili**:**

i. ngazi ya Taifa
ii. ngazi ya Tawi

5. 2 MUUNDO WA UONGOZI NGAZI YA TAIFA

Muundo wa Uongozi utajumuisha;

a. Baraza la Wadhamini,

b. Mwenyekiti wa Chama Taifa,

c. Katibu Mkuu wa chama Taifa,

d. Mweka Hazina wa Chama Taifa

e. Mwenyekiti Kamati ya Wanawake Taifa

f. Katibu Kamati ya wanawake Taifa.

5.2.1 BARAZA LA WADHAMINI

5.2.1.1 WADHAMINI NA KAZI ZAO

Kutakuwa na baraza la Wadhamini litakalokuwa na wajumbe 3 walioteuliwa na kudumu kwa mika mitano (5) Wadhamini wataidhinishwa na kuteuliwa na Mkutano mkuu wa Chama ambao wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

i. Uadilifu na Uzalendo;
ii. Utayari na nia ya kusaidia chama kwa ukaribu;
iii. Wasiwe na madaraka ya kudumu katika Chama;
iv. Wawe wanauelewa wa masuala ya vyama vya wafanyakazi

5.2.1.2 JINSI YA KUWAPATA WADHAMINI

Wadhamini wa Chama wapendekezwa na kamati ya utendaji ya Chama kwa kuzingatia sifa zilizotajwa na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa Chama.

5.2.1.3 KAZI ZA WADHAMINI

Kazi za wadhamini zitakuwa ni hizi zifuatazo:-

i. Kuangalia fedha na rasilimali za chama
ii. Kuangalia hati miliki za mali za chama na utunzaji wake
iii. Kupata nakala na taarifa muhimu za chama kadri zitakavyohitajika
iv. Kufanya kazi chini ya baraza kuu la chama
v. Kulinda siri na taarifa za chama

5.2.1.4 VIKAO VYA BARAZA LA WADHAMINI

i. Baraza la wadhamini litafanya kikao mara moja kwa mwaka
ii. Baraza linaweza kukutana kwa dharura iwapo kuna sababu ya msingi ya kufanya hivyo
iii. Katibu Mkuu wa chama atahakikisha baraza linawezeshwa kufanya vikao vyake kila linapopaswa kufanya hivyo
iv. Baraza litaandaa Muhtasari wa kikao chake na kukiwasilisha kwa katibu Mkuu wa chama
v. Taarifa ya kikao hiki itajadiliwa katika Mkutano Mkuu wa Chama

5.2.1.5 KUJIUZULU UDHAMINI WA CHAMA

i. Mjumbe wa baraza la udhamini anahaki ya kujiuzulu wakati wowote kwa kumuandikia barua ya kujiudhuru Katibu wa chama akielezea sababu za kujiuzulu na kuiwasilisha kwenye Kamati ya utendaji taifa.
ii. Kamati ya utendaji taifa itapeleka barua hiyo kwenye Baraza Kuu kwa maamuzi
iii. Iwapo mdhamini atafariki, kujiuzulu au kuondolewa katika madaraka hayo, nafasi hiyo itajazwa na mdhamini mwingine atakayeteuliwa na Baraza Kuu.
iv. Mdhamini atahesabika kuwa ameondolewa katika shughuli zake iwapo mambo
v. Mdhamini aliyejiuzulu au kuondolewa katika nafasi hiyo kwa utaratibu uliotajwa na Katiba hii, atawajibika kukabidhi hati na mali zote za Chama kwa Katibu Mkuu.

5.2.2. MWENYEKITI WA TAIFA

Kutakuwa na Mwenyekiti wa Taifa ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Chama na kuongoza Chama kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi cha pili cha miaka mitano, na sio zaidi ya vipindi viwili.

5.2.2.1 KAZI ZA MWENYEKITI WA TAIFA

Zifuatazo ndizo kazi za Mwenyekiti wa Taifa:

i. Atakuwa Msemaji Mkuu wa Chama.
ii. Ataongoza vikao vyote vya Kitaifa vya Chama.
iii. Atawajibika katika usimamizi wa nidhamu katika mikutano.
iv. Atatia sahihi katika kumbukumbu za mikutano yote atakayoongoza.
v. Atahakikisha kuwa Katiba na taratibu za Chama zinafuatwa na wale wote wanaohusika.
vi. Katika mikutano anayoiongoza, atakuwa na kura ya turufu licha ya kura yake ya kawaida.

vii. Iwapo atakuwa na udhuru wa kumfanya asiweze kuhudhuria mkutano, mkutano utachagua mwenyekiti kutoka miongoni mwa wajumbe.
viii. Kama kiti cha Mwenyekiti kitabaki wazi kwa sababu yeyote ile kabla ya Mkutano Mkuu wa Chama, Kamati ya Utendaji Taifa itatoa taarifa kwa Baraza Kuu na nafasi hiyo itajazwa na Baraza Kuu la Taifa mpaka Mkutano Mkuu mwingine utakapofanyika.

5.2.3 KATIBU MKUU WA TAIFA

Kutakuwa na Katibu Mkuu wa Chama ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Chama na kushika madaraka kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi cha pili cha miaka mitano, na sio zaidi ya vipindi viwili.

5.2.3.1 KAZI ZA KATIBU MKUU WA TAIFA

Katibu Mkuu wa Taifa atakuwa na kazi zifuatazo:

i. Atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu atakayewajibika katika utekelezaji wa maamuzi mbalimbali na shughuli za kila siku za Chama na atasaidiwa na Manaibu katibu Wakuu waajiriwa wa Chama, mmoja atashughulikia Taasisi za Elimu ya Juu za Umma na mwingine Taasisi za Elimu ya Juu za Binafsi.
ii. Kwa kushauriana na Mwenyekiti wa Taifa, ataitisha vikao vyote vya Chama ngazi ya Taifa.
iii. Atatunza kumbukumbu zote za Chama.
iv. Atakuwa Msimamizi Mkuu wa masuala yote ya Utawala na uratibu kupitia Kamati Kuu.
v. Atasimamia utekelezaji wa mpango wa kazi wa Chama. Aidha, ataandaa taarifa za utendaji kazi za Chama na kuziwasilisha katika vikao husika.
vi. Kwa kushirikiana na Kamati ya Utendaji - Taifa, atapendekeza uteuzi wa watumishi wa Chama kwenye Mamlaka za ajira.
vii. Atafanya shughuli zote za utetezi wa haki na maslahi ya wanachama/wafanyakazi. Kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Chama kwa mujibu wa Katiba hii.
viii. Atatekeleza shughuli zote za Chama kwa kuzingatia katiba ya Chama.

5.2.3.2 NAIBU KATIBU MKUU

Watakuwepo Manaibu Katibu wakuu wawili ambao watakuwa ndio wasaidizi wa Katibu Mkuu Taifa.

5.2.3.2.1 Naibu Katibu Mkuu (Taasisi za Elimu ya Juu za Umma)

Atakuwa mwajiriwa wa mkataba kwa kipindi cha miaka mitano, na endapo utendaji wa kazi zake utaridhisha katika kipindi cha awali, anaweza kuongezewa mkataba mwingine wa miaka mitano, na atakuwa na kazi zifuatazo:

i. Atakuwa Msaidizi na Mshauri Mkuu kwa Katibu Mkuu wa Chama katika masuala yote yahusuyo Taasisi za Elimu ya Juu za Umma.
ii. Atatunza kumbukumbu zote za taasisi anazozisimamia.
iii. Atasimamia utekelezaji wa mpango wa kazi katika eneo lake. Aidha, ataandaa taarifa za utendaji kazi za eneo lake na kuwasilisha kwa Katibu Mkuu.
iv. Atasaidia kufanya shughuli zote za utetezi wa haki na maslahi ya wanachama/wafanyakazi kwa kushauriana na Katibu Mkuu wa Chama kwa mujibu wa Katiba hii na Sheria za nchi.
v. Atafanya kazi nyinginezo atakazopangiwa na Katibu Mkuu.

5.2.3.2.2 Naibu Katibu Mkuu (Taasisi za Elimu ya Juu za Binafsi)

Atakuwa mwajiriwa wa mkataba kwa kipindi cha miaka mitano. Endapo utendaji wa kazi zake utaridhisha katika kipindi cha awali, anaweza kuongezewa mkataba mwingine wa miaka mitano, na atakuwa na kazi zifuatazo:

i. Atakuwa Msaidizi na Mshauri Mkuu kwa Katibu Mkuu katika masuala yote yahusuyo Taasisi za Elimu za Juu za Binafsi.
ii. Atatunza kumbukumbu zote za taasisi zake.
iii. Atasimamia utekelezaji wa mpango wa kazi katika kitengo chake. Aidha, ataandaa taarifa za utendaji kazi za kitengo chake na kushauriana na Katibu Mkuu wa Chama.
iv. Atasaidia kufanya shughuli zote za utetezi wa haki na maslahi ya wanachama/wafanyakazi kwa kushauriana na Katibu Mkuu wa Chama kwa mujibu wa Katiba hii na Sheria za nchi.
v. Atafanya kazi nyinginezo kama atakavyoagizwa na viongozi wakuu wa chama..

5.2.3.2.3 Utaratibu wa Ajira za Manaibu katibu Wakuu

Taratibu zifuatao zitatumika kuwapata Manaibu katibu Wakuu:

i. Kanuni za Utumishi zitaandaliwa na Baraza Kuu na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Chama.
ii. Mapendekezo ya majina ya Manaibu katibu Wakuu yatapelekwa kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya kuidhinishwa na kupitishwa.
iii. Mkutano Mkuu ndicho chombo chenye maamuzi juu ya ajira za Wasaidizi wa Katibu Mkuu.

5.2.4 MWEKA HAZINA

Atakuwepo Mweka Hazina wa Chama ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Chama na kushika madaraka kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza

kuchaguliwa tena kwa kipindi cha pili cha miaka mitano, na sio zaidi ya vipindi viwili.

Mweka Hazina wa Chama atakuwa na wajibu na majukumu ya utunzaji wa kumbukumbu zote za fedha za Chama na atawajibika kutoa taarifa kwa Katibu Mkuu juu ya mapato na matumizi ya fedha za Chama atakapotakiwa kufanya hivyo kwa mujibu wa kanuni za fedha za Chama.

5.2.4.1 KAZI ZA MWEKA HAZINA

i. Ataongoza vikao vyote vya kamati ya fedha;
ii. Kumshauri Katibu Mkuu juu ya masuala yote ya fedha;
iii. Kumshauri Katibu Mkuu juu ya mbinu za kuongeza mapato ya Chama;
iv. Kutunga na kuhakikisha matumizi bora ya fedha kwa kufuata kanuni na taratibu za fedha na sheria za nchi;
v. Atanya kazi zinginezo kama atakavyoelekezwa na viongozi wakuu wa chama na vikao vya kitaifa.

5.2.5 MWENYEKITI KAMATI YA WANAWAKE TAIFA

Kutakuwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake katika ngazi ya Taifa ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Chama na kushika madaraka kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi cha pili cha miaka mitano, na sio zaidi ya vipindi viwili.

5.2.5.1 KAZI ZA MWENYEKITI WA KAMATI YA WANAWAKE TAIFA

i. Atakuwa msemaji mkuu wa kamati
ii. Atamshauri Mwenyekiti wa chama kuhusu sera na masuala mbalimbali yanayomgusa mfanyakazi mwanamke katika mazingira yake ya kazi na maendeleo ya jamii.
iii. Ataongoza vikao vyote vya kamati
iv. Atahamasisha wafanyakazi wanawake kushiriki shughuli za Chama ili kuongeza uelewa wa mwanamke juu ya masuala ya kiajira na kijamii yanayomgusa.
v. Atatia saini katika kumbukumbu za mikutano ya kamati atakayoongoza.

5.2.6 KATIBU KAMATI YA WANAWAKE TAIFA

Kutakuwa na Katibu wa Kamati ya Wanawake ngazi ya Taifa ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Chama na kushika madaraka kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi cha pili cha miaka mitano, na sio zaidi ya vipindi viwili.

5.2.6.1 KAZI ZA KATIBU WA KAMATI YA WANAWAKE TAIFA

i. Ataitisha vikao vya kamati baada ya kushauriana na mwenyekiti wa kamati.
ii. Ataandaa mpango kazi wa kamati.
iii. Atasimamia utekelezaji wa maamuzi ya kamati
iv. Atatunza kumbukumbu za vikao na kazi za kamati.
v. Atashirikiana na mwenyekiti wa kamati kuhamasisha ushiriki wa wafanyakazi wanawake kwenye shughuli za Chama.

5.3 MUUNDO WA UONGOZI NGAZI YA TAWI

Muundo wa Uongozi utajumuisha;

a. Mwenyekiti wa Chama Tawi
b. Katibu wa chama Tawi,
c. Mwenyekiti Kamati ya Wanawake Tawi
d. Katibu Kamati ya wanawake Tawi.

5.3.1 MWENYEKITI WA TAWI

Kutakuwa na Mwenyekiti wa TaWI ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Chama wa Tawi kuongoza Chama katika ngazi ya Tawi kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuchaguliwa tena bila ukomo.

5.3.1.1 KAZI ZA MWENYEKITI WA TAWI

Mwenyekiti wa Tawi atafanya kazi zifuatazo:

i. Atakuwa ndiye Msemaji Mkuu wa Chama katika Tawi.
ii. Atakuwa ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za utendaji katika tawi.
iii. Ataongoza mikutano yote ya Tawi kwa uangalifu na utulivu.
iv. Atatia sahihi katika kumbukumbu za mikutano ya tawi analolisimamia.
v. Atakuwa na kura ya turufu iwapo pande mbili zitagongana, isipokuwa wakati wa uchaguzi

5.3.2 KATIBU WA TAWI

Kutakuwa na Katibu wa Tawi ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Chama wa Tawi na kushika madaraka katika ngazi ya Tawi kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuchaguliwa tena bila ukomo.

.

5.3.2.1 KAZI ZA KATIBU WA TAWI

Katibu wa Tawi atafanya kazi zifuatazo:

i. Atakuwa ndiye Mtendaji wa Halmashauri katika Tawi.
ii. Atawasilisha, kwenye Halmashauri, taarifa za wanachama wote katika Tawi.
iii. Atahudhuria mikutano yote ya Tawi na kutia sahihi na kutunza kumbukumbu zote za chama.
iv. Atatunza vitabu vya hesabu za fedha na hati za Tawi.
v. Ataandaa vikao vyote vya Chama kwa kushauriana na Mwenyekiti.
vi. Atakuwa Katibu wa Vikao vyote vya Chama katika Tawi.
vii. Atawasilisha, katika Halmashauri ya Tawi kila miezi mitatu, taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za Chama pamoja na taarifa za idadi ya Wanachama na maendeleo ya Chama kwa ujumla.

Kama atajiuzulu yeye mwenyewe, au ataacha ukatibu kwa ajili ya sababu zozote zile au atalazimishwa kuacha, atakabidhi kwa Halmashauri ya tawi vitabu na mali za Chama au mauzo ya mali hizo kwa mujibu wa Katiba ya Chama. Kamati ya Halmashauri ya Tawi itamteua Katibu wa muda na kumkabidhi shughuli zote za Chama mpaka uchaguzi utakapofanyika.

5.3.3 MWENYEKITI KAMATI YA WANAWAKE TAWI

Kutakuwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake katika ngazi ya Tawi ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Tawi na kushika madaraka kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuchaguliwa tena bila ukomo.

5.3.3.1 KAZI ZA MWENYEKITI WA KAMATI YA WANAWAKE TAWI

i. Atakuwa mjumbe wa Halmashauri katika Tawi.
ii. Atashughulikia masuala yote ya wanawake katika ngazi ya tawi
iii. Ataitisha vikao vya kamati ya wanawake ngazi ya tawi
iv. Atashiriki katika majadiliano ya pamoja yanayofanyika katika ngazi ya tawi
v. Kwa kushirikiana na Katibu wa Kamati ya Wanawake Tawi atafanya makongamano na maadhimisho yanayohusu wanawake

5.3.4 KATIBU KAMATI YA WANAWAKE TAWI

Kutakuwa na Katibu wa Kamati ya Wanawake ngazi ya Taifa ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Chama na kushika madaraka kwa kipindi

cha miaka mitano na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi cha pili cha miaka mitano, na sio zaidi ya vipindi viwili.

5.3.4.1 KAZI ZA KATIBU WA KAMATI YA WANAWAKE TAWI

i. Ataitisha vikao vya kamati baada ya kushauriana na mwenyekiti wa kamati.
ii. Ataandaa mpango kazi wa kamati.
iii. Atasimamia utekelezaji wa maamuzi ya kamati
iv. Atatunza kumbukumbu za vikao na kazi za kamati.

5.4 VYOMBO VYA MAAMUZI VYA CHAMA

Muundo wa Vyombo vya maamuzi vya chama katika ngazi ya Taifa ni

a. Mkutano Mkuu wa Taifa,

b. Baraza Kuu la Chama

c. Mkutano Mkuu Tawi.

5.4.1 MKUTANO MKUU WA CHAMA WA TAIFA

Kutakuwepo na Mkutano Mkuu wa Chama wa Taifa. Mkutano Mkuu ndicho chombo kikuu cha Chama kitakachokuwa na mamlaka ya juu na ya mwisho katika maamuzi .

5.4.1.1 KAZI ZA MKUTANO MKUU WA CHAMA TAIFA

Mkutano Mkuu wa Chama utafanya kazi zifuatazo:

i. Utapokea na kurekebisha Katiba ya Chama kwa kufuata utaratibu uliowekwa;
ii. Utapitisha sera, kujadili na kuidhinisha kazi za Chama;
iii. Utachambua na kujadili utekelezaji wa mpango wa kazi ulioandaliwa na Baraza Kuu la Chama;
iv. Utakuwa na uwezo wa kuthibitisha, kurekebisha, na kufuta uamuzi wowote uliopitishwa na vyombo vya chini vya Chama au kiongozi yeyote wa Chama;
v. Utatoa uamuzi wa mwisho kuhusu shughuli za uhusiano wa kimataifa na kuhusu Chama kujiunga na Taasisi za Vyama vya Kimataifa na maswala mengine yanayohitaji maamuzi ya kitaifa.

5.4.1.2 HOJA NA MAPENDEKEZO

i. Hoja na mapendekezo mbalimbali yatagawiwa kwa wajumbe wa Mkutano Mkuu kwa maandishi wiki mbili kabla ya Mkutano huo.
ii. Aidha, endapo kikao kitakuwa ni cha dharura, hoja zitagawiwa kwa wajumbe mapema siku ya kikao
iii. Wajumbe watapata fursa ya kuzijadili na kuzikubali ziunganishwe kama agenda za mkutano ulioitishwa.

.

5.4.1.3 VIONGOZI WANAOCHAGULIWA NA MKUTANO MKUU WA CHAMA

Mkutano Mkuu wa Chama utachagua viongozi wafuatao:

i. Mwenyekiti wa Chama wa Taifa;
ii. Katibu Mkuu wa Chama Taifa;
iii. Mwenyekiti Kamati ya Wanawake na ustawi wa jamii Taifa;
iv. Katibu Kamati ya Wanawake na ustawi wa jamii Taifa;
v. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Shirikisho;
vi. Mweka hazina wa chama
vii. Mkutano mkuu pia utathibitisha na kupitisha majina ya wadhamini wa chama

5.4.1.4 WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA CHAMA WA TAIFA

Mkutano Mkuu wa Chama utakuwa na wajumbe wafuatao:

i. Mwenyekiti wa Chama Taifa;
ii. Katibu Mkuu wa Chama Taifa;
iii. Naibu Katibu Mkuu (Taasisi za Elimu ya Juu za Umma);
iv. Naibu Katibu Mkuu (Taasisi za Elimu za Juu za Binafsi);
v. Wenyeviti wote wa matawi;
vi. Makatibu wote wa matawi;
vii. Wadhamini wa chama ambao hawatakuwa na kura;
viii. Mweka Hazina wa Chama;
ix. Mshauri wa Sheria wa chama;
x. Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Wanawake matawini
xi. Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Wanawake Taifa;
xii. Wajumbe wa Kamati ya Utendaji Taifa.
xiii. Wajumbe wengine waliochaguliwa na tawi kwa mujibu wa Katiba kama ilivyoainishwa hapa chini.

5.4.1.5 Uwiano wa Uwakilishi wa Wajumbe kwenye Mkutano Mkuu Taifa Kutoka Matawini

Uwakilishi kutoka matawini katika Mkutano Mkuu Taifa utazingatia idadi ya wanachama katika tawi husika kama ilivyoainishwa hapa chini:

Idadi ya Wanachama Tawini		Idadi ya Wajumbe
10 – 100	-	1
101 – 500	-	2
501 – 1000	-	3
Zaidi 1000	-	4

5.4.1.5 RATIBA YA MKUTANO MKUU WA CHAMA - TAIFA

Mkutano mkuu wa chama utafanyika mara moja kila baada ya miaka miwili.

i. Iwapo kutatokea sababu maalum, Kamati ya Utendaji Taifa ya chama au theluthi mbili za wajumbe wa Baraza la Kuu la chama wanaweza kuamua kuitisha kikao cha Mkutano Mkuu maalum. Mkutano Mkuu maalum utajadili mambo yale tu yaliyosababisha kuitishwa kwa kikao hicho.

ii. Taarifa ya kufanyika kwa Mkutano Mkuu wa Chama itatolewa kwa wajumbe mwezi mmoja kabla ya kikao. Hatahivyo, Taarifa ya muda mfupi inaweza kutolewa kama itabidi kuitisha Mkutano Mkuu maalum.

iii. Akidi ya kufanyika kwa Mkutano Mkuu wa Chama kitakuwa ni theluthi mbili ya wajumbe wote.

iv. Mwenyekiti wa Taifa atakuwa ndiye Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu. Iwapo kwa sababu zozote zile Mwenyekiti atashindwa kuhudhuria, Mkutano Mkuu utachagua Mwenyekiti wa mkutano huo miongoni mwa wajumbe waliohudhuria.

v. Katibu Mkuu wa Taifa atakuwa ndiye Katibu na Mratibu wa Mkutano, na atasaidiwa na manaibu katibu wakuu na kamati ya utendaji Taifa

5.4.2 BARAZA KUU LA CHAMA LA TAIFA

Litakuwa chombo cha pili kimamlaka katika uongozi wa chama baada ya Mkutano Mkuu wa Chama Taifa.

5.4.2.1 KAZI ZA BARAZA KUU LA CHAMA LA TAIFA

i. Kujadili na kutekeleza kazi zote zilizokasimiwa kwake na Mkutano Mkuu;

ii. Kupokea na Kujadili mpango wa kazi wa Kamati ya Utendaji taifaya Chama;
iii. Kuandaa sera ya chama;
iv. Kuhakikisha kwamba shughuli za kamati ya Utendaji - Taifa na Sekretariati zinaendeshwa kwa mujibu wa katiba na matakwa ya wanachama;
v. Kujadili na kupitisha bajeti ya Chama;
vi. Kusimamia nidhamu katika Chama, kusikiliza rufaa toka vyombo vya chini yake na kutoa maamuzi ya mwisho;
vii. Kupokea, kujadili na kuchanganua taarifa mbalimbali za mwaka za shughuli za Chama kama zilivyowasilishwa na Kamati ya Utendaji Taifa;
viii. Kupokea na kujadili taarifa ya kazi za Kamati ya Wanawake na ustawi wa jamii taifa;
ix. Kujadili na kufanya maamuzi juu ya viwango vya mishahara na posho za watumishi na vikao mbalimbali vya Chama;
x. Kujaza nafasi ya ujumbe wa Baraza hilo zinazokuwa wazi baada ya uchaguzi mkuu kwa niaba ya Mkutano Mkuu;
xi. Kuidhinisha pendekezo la Mkaguzi wa Fedha wa Chama;
xii. Kupokea na kuidhinisha ajira za watumishi na uteuzi wa maafisa wa Chama;
xiii. Kuchagua wajumbe wa Baraza Kuu la shirikisho;
xiv. Kuchagua wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya shirikisho.

5.4.2.2 WAJUMBE WA BARAZA KUU

Baraza litakuwa na wajumbe wafuatao:-

i. Mwenyekiti wa Chama wa Taifa;
ii. Katibu Mkuu wa Chama;
iii. Mweka Hazina wa Chama;
iv. Wajumbe ambao ni Mwenyekiti na Katibu wa Tawi kwa mujibu wa Katiba hii;
v. Wadhamini wa Chama ambao hawatakuwa na kura;
vi. Mwenyekiti wa Wanawake - Taifa, Katibu wa Wanawake - Taifa, na wajumbe watatu wa Kamati ya Wanawake ya Taifa;
vii. Mwanasheria wa Chama ambaye hatapiga kura;
viii. Wajumbe wa Kamati ya Utendaji waliopitishwa na Baraza Kuu;
ix. Wajumbe wa kuchaguliwa kutoka kila tawi kwa mujibu wa katiba hii;
x. Manaibu Katibu Wakuu wasaidizi wa Chama ambao hawatapiga kura.

5.4.2.3 Uwiano wa Uwakilishi wa Wajumbe kwenye Baraza Kuu Kutoka Matawini

Uwakilishi kutoka matawini katika Baraza Kuu itazingatia idadi ya wanachama katika tawi husika kama ilivyoainishwa hapa chini:

Idadi ya Wanachama Tawini		Idadi ya Wajumbe
10 – 300	-	1
301 – 600	-	2
Zaidi – 600	-	3

5.4.2.4 VIKAO VYA BARAZA KUU

Ufuatao ndio utaratibu wa vikao vya Baraza Kuu:

i. Baraza Kuu la Taifa litakutana mara moja kwa mwaka**.**
ii. Kamati ya Utendaji taifa inaweza kuitisha kikao maalum cha Baraza Kuu iwapo theluthi moja ya wajumbe wa Baraza Kuu la Chama wametaka hivyo kwa maandishi.
iii. Taarifa na tarehe ya mkutano itatolewa mwezi mmoja kabla ya Kikao hicho. Taarifa fupi inaweza ikatolewa kwa ajili ya kikao maalum cha Baraza Kuu la Chama.
iv. Mwenyekiti wa Chama ndiye atayekuwa Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Chama la Taifa. Mwenyekiti asipohudhuria Mkutano kwa sababu zozote zile, wajumbe wa Baraza Kuu watachagua Mwenyekiti miongoni mwao ili kuongoza mkutano huo.

5.4.3 MKUTANO MKUU WA WANACHAMA WA TAWI

Mkutano Mkuu wa wanachama wote wa tawi utafanyika mara moja kwa mwaka au wakati wowote inapotokea dharura. Kazi zake ni kama ifuatavyo:

i. Kupokea na kujadili tathmini ya utekelezaji wa mpango wa kazi;
ii. Kupokea na kujadili tathmini ya utekelezaji wa kanuni za afya na usalama kazini;
iii. Kupokea na kujadili tathmini ya utekelezaji wa mazingira ya kazi na ajira
iv. Kupokea na kujadili hali ya wastaafu na kutoa mapendekezo ya kuboresha mazingira kazi ya wastaafu;
v. Kupokea na kujadili mapendekezo ya mkataba wa hali bora;
vi. Kupokea na kujadili ustawi wa ajira na vikwazo vinavyotoka na mabadiliko ya uchumi na kutoa mapendekezo;
vii. Kupokea na kujadili ushauri wa kamati mbalimbali za wataalamu juu ya masharti ya kazi na mazingira yake;
viii. Kupokea taarifa ya maamuzi mbalimbali ya taasisi;

ix. Kupokea na kujadili taarifa ya halmashauri ya tawi na kutolea maamuzi;
x. Kupokea na kujadili njia za kutekeleza maamuzi yaliyopitishwa na ngazi mbalimbali za chama za kamati mbalimbali za Halmashauri za tawi;
xi. Kupokea na kujadili mpango wa kazi wa Tawi.

5.4.4 MKUTANO WA WANACHAMA WA TAWI

i. Tawi litafanya vikao vyake mara mbili kwa mwaka
ii. Wajumbe wa mkutano wa wanachama watakuwa ni wanachama wote wa Tawi husika
iii. Kikao kitaitishwa na katibu wa Tawi baada yakushauriana na Halmashauri ya Tawi na Mwenyekiti wa Tawi.
iv. Katibu atatoa notisi ya kufanyika kwa kikao kwa wajumbe ndani ya siku 14
v. Wajumbe watapata fursa ya kutoa agenda zao ili zijumuishwe kwenye agenda za kikao husika
vi. Katibu wa Tawi atatakiwa kuwasilisha Muhtasari wa kikao kwa Katibu Mkuu wa chama Taifa ndani ya siku 21 tangu tarehe ya kufanyika kwa kikao husika.

5.4.5 MKUTANO WA WAFANYAKAZI WOTE

i. Halmashauri ya tawi itaitisha Mkutano wa Wafanyakazi wote mara mpja kwa mwaka
ii. Halmashauri ya Tawi itatoa notisi ya kufanyika kwa Mkutano huo ndani ya siku 14.
iii. Wajumbe wa Mkutano huo ni wafanyakazi wote bila kujali uanachama wao katika chama chochote cha wafanyakazi
iv. Mkutano utaongozwa na Mwenyekiti wa Tawi
v. Katibu wa Tawi ataandika muhtasari wa kikao
vi. Muhtasari wa kikao hicho utatumwa kwa Katibu Mkuu wa Chama Taifa na kwa Mwajiri ambapo Tawi husika limeundwa.

5.4.5.1 KAZI ZA MKUTANO WA WAFANYAKAZI WOTE

Mkutano wa Wafanyakazi wote katika Tawi utafanyika mara moja kwa mwaka na utafanya kazi zifuatazo:

i. Kujadili utekelezaji mkataba wa hali bora kama ulivyowasilishwa na Halmashauri ya Tawi na mwajiri;
ii. Kujadili taarifa ya utendaji wa Baraza la Wafanyakazi;
iii. Kujadili utekelezaji wa mipango mbalimbali ya ustawi wa ajira na mazingira ya kazi;
iv. Kujadili uboreshaji wa masharti ya utumishi;

v. Kujadili ufanisi na utendaji wa Kamati za Afya na Usalama kazini.

5.5 KAMATI ZA UTENDAJI ZA CHAMA

Kutakuwa na kamati za utendaji katika ngazi ya Taifa na Matawi ambazo zitakuwa zinaratibu mwendo wote wa shughuli za kazi za Chama katika ngazi husika . Kamati hizi zitajumisha

a. Kamati ya Utendaji Taifa
b. Kamati ya Wanawake ngazi ya Taifa na Tawi
c. Halimashauri ya Tawi

5.5.1 KAMATI YA UTENDAJI TAIFA YA CHAMA

5.5.1.1 WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI TAIFA YA CHAMA

Wajumbe wa Kamati ya Utendaji watakuwa kama ifuatavyo:

i. Katibu Mkuu wa Chama ambaye atakuwa ni Mwenyekiti;
ii. Naibu Makatibu Wakuu ;
iii. Katibu wa Kamati ya Wanawake na ustawi wa jamii– Taifa, ambaye ndiye atakuwa katibu wa kamati;
iv. Mweka Hazina wa Chama;
v. Wajumbe wasiozidi Sita watakaopendekezwa na Katibu Mkuu na kuthibitishwa na Baraza Kuu;
vi. Mwanasheria wa Chama.

Kamati inaweza kuunda kamati ndogo za kitaalamu kulingana na mahitaji ya wakati husika.

5.5.1.2 KAZI NA MAJUKUMU YA KAMATI YA UTENDAJI TAIFA

Kamati ya utendaji itakuwa na kazi na majukumu yafuatayo:

i. Kuratibu mwenendo wote wa shughuli na kazi za Chama;
ii. Kupokea na kupendekeza majina katika nafasi mbalimbali za utumishi za kitaifa;
iii. Kumshauri Katibu Mkuu juu ya masuala yote yahusuyo uendeshaji wa Chama;
iv. Kuandaa vikao vya Baraza Kuu;

v. Kuandaa mpango wa kazi za Chama, taarifa ya fedha, bajeti ya Chama na kuiwasilisha kwenye Baraza Kuu;
vi. Kuhakikisha kwamba utendaji kazi wa Chama unafanywa kwa kuzingatia Katiba na unakidhi matarajio na matakwa ya wanachama;
vii. Kuandaa na kuwasilisha, kwenye Baraza Kuu, Kanuni za Fedha za Chama;
viii. Kuidhinisha michango kwa shughuli maalum;
ix. Kubuni, kuandaa na kuwasilisha kwenye Baraza Kuu Mipango/Sera na Programu zote za uboreshaji na uendeshaji wa Chama;
x. Kutoa mapendekezo kuhusu maslahi ya viongozi na watumishi wa Chama katika maeneo yafuatayo:
- Miundo ya Utumishi na ngazi za mishahara;
- Kanuni/masharti ya Utumishi.
xi. Kudhibiti mapato na matumizi ya fedha ya Chama;
xii. Kufanya marekebisho ya matumizi ya fedha katika kasma yoyote ile inapolazimu;
xiii. Kupendekeza uteuzi wa watumishi wa Idara za Chama;
xiv. Kupendekeza Mkaguzi wa Mahesabu wa Chama kwenye Baraza Kuu la Chama;
xv. Kupokea na kutolea uamuzi mapendekezo yote ya wanachama toka matawini

5.5.1.3 MIKUTANO YA KAMATI YA UTENDAJI YA TAIFA

Kamati ya Utendaji itakutana mara moja kila baada ya miezi mitatu. Kamati ya Utendaji inaweza kukutana wakati wowote inapotokea dharura.

5.5.2 KAMATI ZA WANAWAKE ZA CHAMA

Kutakuwepo Kamati za Wanawake katika ngazi ya Tawi na Taifa. Kamati hizi itawajibika kwa chombo kikuu cha utendaji katika ngazi husika.

5.5.2.1 KAMATI YA WANAWAKE -TAIFA

Katika ngazi ya taifa, kutakuwepo viongozi watano ambao ni Mwenyekiti - Taifa, Katibu - Taifa na wajumbe watatu watakaoteuliwa na katibu Mkuu wa chama baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake na Ustawi wa jamii Taifa kisha kuidhinishwa na baraza kuu. Vilevile, kutakuwa na wajumbe wa Kamati ya Wanawake - Taifa watakaochaguliwa kutoka tawi.

5.5.2.1.1 KAZI ZA KAMATI YA WANAWAKE - TAIFA

Kazi za Kamati ya Wanawake -Taifa itakuwa ni:

i. Kupata takwimu za kitafiti zinazochambua mazingira kazi wanayokabiliana nayo wanawake;
ii. Kuwaelimisha wanawake kuhusu wajibu na umuhimu wa kamati za wanawake matawini;
iii. Kutumia takwimu za kitafiti kuandaa mapendekezo na program za kuondoa mazingira hatarishi katika ajira za mfanyakazi mwanamke;
iv. Kubuni mbinu mbalimbali ili kuwawezesha wanawake kushiriki katika uongozi katika ngazi zote, kuongeza kipato na kuboresha mazingira/makazi;
v. Kuratibu mapendekezo yanayotoka ngazi za chini;
vi. Kuwa na kumbukumbu na takwimu mbalimbali juu ya wafanyakazi wanawake kitaifa;
vii. Kamati ya Wanawake Taifa itakutana kabla ya vikao vya Baraza Kuu;
viii. Kuratibu shughuli za maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kitaifa.

Kushiriki katika shughuli mbalimbali za kuhamasisha wanawake katika uchangiaji wa maendeleo ya jamii.

5.5.2.2 KAMATI YA WANAWAKE - TAWI

Viongozi na wajumbe wote wa kamati ya Wanawake ngazi ya tawi watachaguliwa na mkutano mkuu wa uchaguzi ngazi ya tawi.

5.5.2.2.1 UWIANO WA WAJUMBE KATIKA KAMATI ZA WANAWAKE TAWI

Uundaji wa Kamati ya Wanawake, katika ngazi ya tawi utazingatia uwiano wa wanachama katika tawi husika.

1. Tawi Lenye Wanachama 10 – 50

i. Kamati ya wanawake itakuwa na wajumbe watatu: Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina.
ii. Mwenyekiti atakuwa mjumbe wa Halmashauri ya tawi.

2. Tawi Lenye Wanachama 51–100

i. Kamati itakuwa na wajumbe wanne (4) ambao ni pamoja na waliotajwa katika kifungu (9.1.1) hapo juu.
ii. Mwenyekiti atakuwa mjumbe wa Halmashauri ya tawi.

3. Tawi Lenye Wanachama 100 – 500

i. Kamati itakuwa na wajumbe watano (5) ambao ni pamoja na waliotajwa katika kifungu (9.1.1).
ii. Mwenyekiti na katibu watakuwa wajumbe wa Halmashauri ya tawi.

4. Tawi Lenye Wanachama 500 – 1000

i. Kamati itakuwa na wajumbe sita (6) ambao ni pamoja na waliotajwa katika kifungu (9.1.1).
ii. Mwenyekiti na katibu watakuwa wajumbe wa Halmashauri ya tawi.

5. Tawi Lenye Zaidi ya Wanachama 1000

i. Kamati itakuwa na wajumbe saba (7) ambao ni pamoja na waliotajwa katika kifungu (9.1.1).
ii. Mwenyekiti na katibu watakuwa wajumbe wa Halmashauri ya tawi.

5.5.2.2.2 KAZI ZA KAMATI YA WANAWAKE TAWINI

(i). Kuratibu shughuli za wanawake tawini na maadhimisho mbalimbali ya wanawake katika ngazi ya tawi;
(ii). Kupata takwimu za kitafiti zinazochambua mazingira kazi wanayokabiliana nayo wanawake;
(iii). Kuwaelimisha wanawake kuhusu wajibu na umuhimu wa Kamati ya Wanawake tawini;
(iv). Kutumia takwimu za kitafiti kuandaaa mapendekezo na programu za kuondoa mazingira hatarishi katika ajira ya mfanyakazi mwanamke tawini.
(v). Kubuni mbinu mbalimbali za kuongeza kipato cha wanawake na kuboresha mazingira ya kazi tawini.
(vi). Kuratibu mapendekezo yanayotoka kwa wanawake tawini na kuwasilisha katika vikao vya Halmashauri ya tawi.

5.5.2.3 VIKAO VYA KAMATI YA WANAWAKE

(i). Kamati ya wanawake ngazi ya Taifa itakutana angalau mara mbili (2) kwa mwaka.
(ii). Kamati ya wanawake ngazi ya tawi itakutana mara nne (4) kwa mwaka.
(iii). Kamati ya wanawake tawini itakutana na wanawake wote wanachama tawini mara moja (1) kwa mwaka.
(iv). Mkutano Mkuu wa wanawake utafanyika mara moja (1) kwa mwaka.
(v). Kamati ya wanawake Taifa itakutana kabla ya vikao vya Baraza Kuu.

5.5.2.4 WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA KAMATI YA WANAWAKE TAIFA

i. Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake –Taifa
ii. Katibu wa Kamati ya Wanawake –Taifa
iii. Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Wanawake Tawi
iv. Mjumbe wa Kuchaguliwa wa Mkutano mkuu wa Wanawake Tawi

5.5.3 HALMASHAURI YA TAWI NA KAZI ZAKE

5.5.3.1 WAJUMBE WA HALMASHAURI

Halmashauri ya Tawi itaundwa na Mwenyekiti na Katibu wa tawi , mwenyekiti na katibu wa kamati ya wanawake ngazi ya tawi pamoja na wawakilishi wa tawi.

Uwiano wa uwakilishi wa wajumbe wa Halmshauri ya Tawi itakuwa kama ifuatavyo:

i. Wawakilishi 3 kwa Wanachama kumi mpaka ishirini

ii. Wawakilishi kumi (10) wa Tawi kwa Wanachama ishirini na moja mpaka mia moja

iii. Wawakilishi kumi na watano (15) kwa Wanachama zaidi ya mia

iv. Uwakilishi huu utazingatia Jinsia na idadi sawa ya wajumbe.

5.5.3.2 WAJUMBE MAHALA AMBAPO HAKUNA TAWI LA CHAMA

Mahali pa kazi ambapo idadi ya wanachama hawafiki 10 utaratibu wa uwakilishi utafanyika kwa tawi lililopo karibu na sehemu hiyo ya kazi. Aidha mwakilishi mmoja atachaguliwa na atakuwa mjumbe katika halmashauri ya tawi.

5.5.3.3 KAZI ZA HALMASHAURI YA TAWI

Kazi kuu za halmashauri ni:

i. Kuitisha vikao vya Tawi kadri katiba inavyoelekeza
ii. Kulinda, kutetea na kuendeleza haki na maslahi ya wanachama wake na kuhakikisha kuwa afya na usalama vinadumishwa mahali pa kazi;

iii. Kuandaa na kuwasilisha mikataba ya hali bora za kazi kwa kushirikiana na uongozi wa chama ngazi ya Taifa na kuiwasilisha kwenye vikao vya majadiliano na mwajiri;
iv. Kushauriana na Mwajiri juu ya njia za kukuza tija na kuendeleza uzalishaji na ajira ya uhakika, masuala ya hifadhi ya jamii na kuhakikisha kuwa wanachama wanafaidika kutokana na ziada inayotokana na ongezeko la tija;
v. Kutoa taarifa ya shughuli za Chama kwa wanachama na kwenye uongozi wa Chama ngazi ya Taifa
vi. Kuandaa mikutano ya tawi kwa mujibu wa katiba hii;
vii. Kuunda kamati mbalimbali kwa ajili ya ufanisi na utendaji wa kazi zake kwa mujibu wa katiba.
viii. Kuhakikisha kuwa taarifa ya fedha ya tawi inaandaliwa na kuwasilishwa kwa wanachama kwa mujibu wa miongozo na kanuni za Chama.
ix. Kuwasilisha taarifa ya mapato na matumizi kwa Makao Makuu ya Chama kila mwishoni mwa mwaka husika.
x. Tawi litatekeleza majukumu yake kwa kuwasilina na kutoa taarifa Makao Makuu ya Chama katika kila jukumu inalotekeleza.

5.5.3.4 Vikao vya Halmashauri ya Tawi.

Mkutano wa Halmashauri ya Tawi utafanyika kabla ya Mkutano wa wanachama wa Tawi ili kufanya tathmini ya awali juu ya utekelezaji wa maelekezo au maagizo ya Mkutano Mkuu wa Tawi. Mkutano utatafuta njia nzuri zaidi ya kufanikisha utekelezaji kabla ya muda wa utekelezaji husika kuisha.

Halmashauri ya Tawi itafuata utaratibu ufuatao:-

i. Halmashauri ya Tawi itaitisha Mkutano wa wanachama wote.
ii. Tawi litafanya Vikao vyake mara moja kila baada ya miezi mitatu. Hata hivyo, kikao cha dharura kwa kadri uhitaji utakavyotokea kinaweza kuitishwa.
iii. Mwenyekiti wa Tawi ndiye atakayeongoza mikutano yote ya Halmashauri ya Tawi. Endapo Mwenyekiti wa Tawi atakuwa na udhuru wa kumfanya asihudhurie vikao wajumbe watamchagua miongoni mwao mjumbe mmoja kuwa Mwenyekiti wa kikao.
iv. Endapo wanachama wa tawi husika wanapiga kura ya kutaka kuitishwa kwa mgomo kwa mujibu wa Sheria ya ajira na mahusiano kazi Na 6/2004 Chama kitaitisha mgomo.

SEHEMU YA SITA

6.0 TARATIBU ZA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA CHAMA

Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Uchaguzi katika ngazi zifuatazo

a. Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa Taifa
b. Mkutano Kuu wa Uchaguzi Tawi

6.1 MKUTANO MKUU WA UCHAGUZI WA TAWI

Kutakuwepo uchaguzi ngazi ya Tawi. Uchaguzi huo utafanyika kwa mujibu wa Sheria, Katiba ya Chama pamoja na kanuni zake.

i. Tawi litakuwa na Mkutano Mkuu wa Uchaguzi utaofanyika baada ya utaratibu wa kuanza kufanyika kwa uchaguzi kutolewa na Makao Makuu ya chama.
ii. Mkutano utachagua wajumbe wasiopungua watatu na wasiozidi watano kuunda kamati ya usimamizi ya uchaguzi
iii. Wajumbe watakao chaguliwa kuunda kamati ya usimamizi wa uchaguzi hawataruhusiwa kugombea nafasi yeyote kwa husika.
iv. Kikao kitachagua kamati ya usimamaizi ya uchaguzi ambayo itawajibika kuhakiki wagombea wa nafasi mbalimbali za uchaguzi katika ngazi ya tawi kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi zitakazowekwa na chama.
v. Kikao kitashirikisha wanachama wote katika mchakato mzima wa uchaguzi.
vi. Kikao kitaandaa muhtasari wake na kuuwasilisha Makao Makuu ya chama ndani ya sku 21 tangu kufanyika kwa mkutano husika.
vii. Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa Tawi utachagua wajumbe katika nafasi zifuatazo: Viongozi wa tawi; Viongozi wa Kamati ya Wanawake tawi; Wajumbe wa Halmashauri ya tawi; Wajumbe wa Baraza Kuu Taifa; Wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa; Wajumbe wa Kamati ya Wanawake Taifa.

6.1.1 MASHARTI YA KUSHIRIKI UCHAGUZI

i. Ni Wanachama hai tu ndio watakaoruhusiwa kushiriki katika kikao cha uchaguzi.
ii. Ni Wanachama hai tu ndio watakuwa na haki ya kupiga kura na kuchaguliwa katika uongozi wa ngazi mbalimbali za Chama.

6.1.2 KAMATI YA USIMAMIZI YA UCHAGUZI

i. Kamati ya Usimamizi ya Uchaguzi itaundwa na mamlaka husika na itakuwa na wajumbe wasiopungua watatu na wasiozidi watano kati yao

awepo mjumbe mwanamke, watakaochaguliwa kwa kipindi cha mwaka mmoja.

ii. Wajumbe wa Kamati ya usimamizi ya uchaguzi iliyopita, wanaweza kuchaguliwa kama wajumbe wa Halmashauri ya Tawi ingawa wajumbe wa Halmashauri ya Tawi hawaruhusiwi kuwa wajumbe wa Kamati mpya ya usimamizi ya Uchaguzi.

iii. Mapendekezo yote ya wagombea yatawasilishwa na Kamati ya Usimamizi ya uchaguzi ya Tawi kwenye Mkutano Mkuu wa uchaguzi wa Tawi wiki tatu kabla ya tarehe ya uchaguzi.

6.1.3 KAZI ZA KAMATI YA USIMAMIZI WA UCHAGUZI

Kazi za Kamati ya Usimamizi wa Uchaguzi zitakuwa:

i. Kuhakikisha kuwa kuna mapendekezo ya kutosha katika nafasi zote za wagombea;
ii. Kuhakikisha kwamba ni wanachama hai tu ndio walioruhusiwa kuingia na kushiriki katika kikao cha Mkutano Mkuu wa uchaguzi;
iii. Kusikiliza rufaa zitokanazo na uchaguzi husika;
iv. Kutunza nyaraka za matokeo yote ya uchaguzi mpaka muda wa rufaa, kwa mujibu wa katiba hii, utakapoisha.
v. Kuandaa taarifa rasmi ya uchaguzi na kuiwasilisha makao makuu ya chama ndani ya wiki mbili baada ya uchaguzi kufanyika.
vi. Kusimamia makabidhiano ya uongozi na taarifa ya makabidhiano iwasilishwa kwa maandishi makao makuu ya chama.

Pamoja na uwepo wa kamati ya usimamizi wa uchanguzi tawi, uchaguzi huo pia utashuhudiwa na uwakilishi wa chama ngazi ya taifa.

6.1.4 UKOMO WA UONGOZI

i. Wajumbe wa Halmashauri ya Tawi pamoja na Mwenyekiti na Katibu wa Tawi watachaguliwa kila baada ya miaka mitano (5)
ii. Baada ya ukomo wa viongozi wa tawi wa miaka mitano, uchanguzi wa viongozi wa tawi unapaswa kufanyika ndani ya mwezi moja kabla au baada ya ukomo huo.
iii. Endapo muda wa Viongozi wa tawi kupita kwa zaidi ya miezi miwili, Viongozi wa tawi husika utakuwa ni batili. Utaratibu wa baada ya ukiukwaji wa muda wa uongozi utaelekezwa kwenye kanuni za uongozi wa Chama.

6.2 UCHAGUZI NGAZI YA TAIFA

Kutakuwepo uchaguzi wa Viongozi ngazi ya Taifa utakaofanyika kila baada ya miaka mitano utakoendeshwa na Mkutano Mkuu Maalumu wa Uchaguzi. Uchaguzi huo utafanyika kwa mujibu wa Sheria, Katiba ya Chama pamoja na kanuni zake.

6.2.1 MASHARTI YA KUSHIRIKI UCHAGUZI

i. Mgombea wa nafasi yeyote ile, isipokuwa watumishi wa chama na maafisa wa kuteuliwa, atajaza fomu ya maombi ya uongozi na kuipitisha katika tawi lake katika Kamati ya Usimamizi ya uchanguzi ya tawi lake;
ii. Mgombea wa nafasi yoyote katika ngazi ya taifa yaani Mwenyekiti wa taifa, Katibu Mkuu, Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake - Taifa na Katibu wake, lazima adhaminiwe na wanachama kutoka tawi lake na matawi mengine nje ya Taasis yake. angalau wawili kutoka kila tawi;
iii. Majina yote ya wagombea yatapokelewa na Kamati ya usimamizi ya uchaguzi;
iv. Kamati ya Utendaji taifa itatengeneza kanuni za uchaguzi za kila ngazi ya uongozi;
v. Kamati ya usimamizi ya uchaguzi katika ngazi ya taifa itachaguliwa na mkutano wa Baraza kuu la chama.
vi. Wajumbe wa kamati ya uchaguzi hawatakuwa wagombea wa nafasi yoyote katika uchaguzi huo.

6.2.1 Utaratibu wa kupiga kura

Utaratibu wa kupiga kura ni kama ifuatavyo:

i. Uchaguzi utafanyika kwa kura ya siri.
ii. Mwenyekiti wa taifa atalazimika kupata zaidi ya nusu ya kura zilizopigwa lakini kwa nafasi zingine zote wingi wa kura utazingatiwa.
iii. Katibu Mkuu wa Chama - Taifa atalazimika, pia, kupata zaidi ya nusu ya kura zilizopigwa.
iv. Maamuzi mengine yoyote ya Mkutano Mkuu yatapitishwa kwa zaidi ya nusu ya kura zilizopigwa na wajumbe waliopiga kura.
v. Mabadiliko yoyote katika Katiba ya Chama, yatapitishwa kwa theluthi mbili ya kura za wajumbe wote wa Mkutano Mkuu kwa mujibu wa katiba iliyopo.

SEHEMU YA SABA

7.0 KAMATI MBALIMBALI ZA CHAMA

7.1 KAMATI YA MAADILI NA UTAWALA BORA YA CHAMA

Kutakuwepo na Kamati ya Maadili ya Chama itakayosimamia maadili na mwenendo wa viongozi pamoja na wanachama katika ngazi zote.

7.1.1 WAJUMBE WA KAMATI YA MAADILI

Kamati hii itaundwa na wajumbe watano **au wasiozidi tisa** watakaoteuliwa na Mwenyekiti wa Chama - Taifa akishirikiana na Katibu Mkuu na kupitishwa na Baraza kuu laChama. Kamati hii itadumu kwa miaka mitatu baada ya kuteuliwa lakini wajumbe wake wanaweza kuteuliwa tena lakini si zaidi ya mara mbili.

7.1.2 KAZI ZA KAMATI YA MAADILI

Kamati itakuwa na kazi zifuatazo:

i. Kusimamia maadili ya viongozi katika ngazi zote;
ii. Kuandaa kanuni zitakazoleta misingi ya utawala bora katika Chama;
iii. Itapokea matatizo yake yote kupitia kamati ya Utendaji Taifa;
iv. Kusikiliza mashauri yote yahusuyo maadili na kutoa mapendekezo yake kwenye Baraza Kuu na Mkutano Mkuu.
v. Kutoa elimu ya utawala bora kwa viongozi na wanachama kwa ujumla.
vi. Kuhakikisha kwamba chama kinaongozwa kwa kufuata misingi ya utawala bora.

7.2 KAMATI ZA USHAURI YA CHAMA

Kutakwepo na Kamati za Ushauri ya Chama kwa lengo mahususi la kumshauri Mwenyekiti wa Chama - Taifa kwa mambo au masuala ya dharura yahusuyo Chama.

7.2.1 WAJUMBE WA KAMATI YA USHAURI

Kamati hii itakuwa na wajumbe wasiopungua watano na wasiozidi kumi watakaoteuliwa na Mwenyekiti wa Chama - Taifa. Kamati hii itaitishwa muda wowote jambo la dharura litakapojitokeza na itaongozwa na Mwenyekiti wa Chama - Taifa. Kazi za kamati hii ni hizi zifuatazo:

i. Kumshauri mwenyekiti wa Chama - Taifa juu ya jambo lolote la dharura;
ii. Kujadili na kupendekeza hatua za dharura za kuchukuliwa inapobidi;
iii. Kupokea na kufanyia kazi mapendekezo yanayohitaji utekelezaji wa haraka kutoka kwenye matawi.

SEHEMU YA NANE

8.0 MAPATO YA CHAMA

8.1 UPATIKANAJI WA FEDHA

Chama kitaendesha shughuli zake kutokana na mapato yatayotokana na ada ya kila mwezi, misaada kutoka kwa wafadhili/wahisani, miradi ya uchumi ya Chama, misaada kutoka kwa vyama rafiki vya wafanyakazi, Taasisi za Fedha na watu binafsi. Mapato hayo yatatumika kwa mujibu wa kanuni za fedha na utaratibu uliowekwa na Katiba hii.

8.2 KANUNI ZA MATUMIZI YA FEDHA

Kufuatana na masharti ya Katiba hii, kutakwepo na Kanuni za Fedha (Financial Regulations) za Chama ambazo zitaongoza namna ya kusimamia, kutunza na kutumia fedha na mali za chama. Kamati ya Utendaji au Halmashauri ya Tawi zitakuwa ndizo zenye mamlaka ya kutoa idhini ya kufungua Akaunti za Benki kwa jina la THTU. Kanuni za Chama zitaelekeza kiwango cha mapato ya Chama kwa asilimia, ngazi ya taifa na tawi, kitakachopaswa kutengwa kwa ajili ya shughuli za Kamati ya Wanawake.

8.3 UKAGUZI WA FEDHA NA MALI ZA CHAMA

i. Hesabu za fedha na mali za Chama - Kitaifa zitakaguliwa mara moja kwa mwaka na Mkaguzi mahsusi aliyeteuliwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Taifa.
ii. Taarifa za wanachama pamoja na mahesabu yaliyokaguliwa, yatapelekwa kwenye mkutano mkuu kwa ajili ya kuidhinishwa na kupitishwa.
iii. Taarifa za wanachama pamoja na mahesabu zitawasilishwa kwa Msajili wa Vyama Huru vya Wafanyakazi na Waajiri kwa mujibu wa kifungu Na. 51 na 52 vya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004.
iv. Katibu mkuu atafuatilia na kukagua matumizi ya fedha za chama ngazi ya tawi kwa kila mwaka.

SEHEMU YA TISA

9.0. UTUMISHI KATIKA CHAMA

Chama kitaajiri watumishi kwa utaratibu utakaowekwa na vikao halali vya Chama. Kutakuwa na miundo na Kanuni za Utumishi ambazo zitaongoza namna ya kusimamia na kutekeleza maslahi na maendeleo ya Watumishi wa Chama.

Chama kwa kupitia katibu mkuu kitateua kamati ya Rasilimali watu itakapobidi ili kupitia maslahi mbalimbali ya viongozi na watumishi wa chama.

Kamati ya Rasilimali watu itatoa taarifa yake kwa kamati ya Utendaji Taifa kabla ya hoja kuwasilishwa kwenye mkutano wa Baraza kuu kwa majadiliano na kuidhinisha au vinginevyo.
Ikama ya Chama itatayarishwa na Kamati ya Rasilmali na kuwasilishwa kwenye Kamati ya Utendaji kupitishwa na Baraza Kuu.

SEHEMU YA KUMI

10. MENGINEYO

10.1 KIWANGO CHA MAHUDHURIO YA MIKUTANO

Bila kuathiri yaliyomo katika baadhi ya vifungu vya Katiba hii, kiwango cha mahudhurio kwa mikutano yote ya Chama itakuwa ni nusu ya wajumbe wanaotakiwa kuhudhuria mkutano huo isipokuwa mkutano wa kubadili katiba akidi ifikie theluthi mbili ya wajumbe wa mkutano mkuu.

10.2 NAFASI KUWA WAZI

Mjumbe wa chombo chochote cha maamuzi katika Chama ataacha kuwa mjumbe na nafasi yake itatangazwa kuwa iko wazi baada ya mojawapo ya haya yafuatayo kutokea:

i. Akihama Chama.

ii. Akiachishwa uanachama kwa mujibu wa Katiba hii.

iii. Akiacha uongozi kwa mujibu wa Katiba hii.

iv. Akikosa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo bila sababu za kuridhisha.

v. Akifariki dunia.

vi. Akiacha kazi.

10.3 KUJAZA NAFASI ZILIZO WAZI

Kila nafasi itakapoachwa wazi katika Chama, mamlaka inayohusika itaijaza mapema iwezekanavyo hiyo kwa mujibu wa Katiba hii.

10.4 KUJIUZULU UONGOZI

i. Kiongozi wa Chama anayetaka kujiuzulu, anaweza kufanya hivyo kwa kuandika barua kwa mamlaka husika.

10.5 KUJITOLEA KWA AJILI YA CHAMA

Viongozi na Maafisa wote wa Chama watajitolea wakati wote kukitumikia chama kwa maslahi ya wanachama.

10.6 KUSIMAMISHWA UONGOZI

i. Kiongozi yeyote wa kuchaguliwa atakayefanya mambo kinyume cha Katiba ya Chama, atasimamishwa uongozi na mamlaka husika.

ii. Viongozi waliochaguliwa na Mkutano Mkuu waTaifa, watasimamishwa uongozi na Baraza Kuu la Taifa, lakini watakuwa na haki ya kuomba rufaa kwenye Mkutano Mkuu wa Taifa. Bila kuathiri maelekezo hayo, uamuzi wa kusimamishwa na Baraza Kuu utakuwa na nguvu na utaanza kazi mara moja mpaka Mkutano Mkuu utakapoamua vinginevyo.

iii. Kiongozi mwingine yeyote aliyechaguliwa au kuteuliwa, atasimamishwa na mamlaka iliyomchagua au kumteua na atakuwa na haki ya kuomba rufaa katika mamlaka ya juu inayofuatia bila kuathiri haki hiyo. Uamuzi wa mamlaka iliyomsimamisha, utaanza kazi mara moja na utakuwa na nguvu mpaka uamuzi wa mamlaka ya juu utakapoamua vinginevyo.

10.7 KUACHISHWA/KUSIMAMISHWA UONGOZI

Kiongozi yeyote wa Chama anaweza kuachishwa au kusimamishwa uongozi na mamlaka iliyomchagua.

10.8 MAHUDHURIO YA MIKUTANO

Mjumbe wa mamlaka yoyote katika Chama aliyewekwa kwa mujibu wa Katiba hii, ataacha kuwa mjumbe kama atashindwa kuhudhuria mikutano mitatu mfululizo bila sababu za kuridhisha kwa mamlaka inayohusika.

10.9 TARATIBU ZA UCHAGUZI

i. Kila mwanachama hai ana haki ya kuchaguliwa kuwa mjumbe katika vyombo vya Chama katika ngazi yoyote ya Chama.

ii. Uchaguzi, katika ngazi zote za Chama, utafanyika kwa mujibu wa kanuni, taratibu na mwongozo wa uchaguzi wa Chama.

10.10 KUJIDHIHIRISHA KWA VIONGOZI

i. Viongozi na watendaji wote wa Chama watawajibika kukitumikia Chama kwa uadilifu na uaminifu wa hali ya juu na hawatakiwi kujiingiza katika shughuli ambazo zinapingana na shughuli za Chama.

ii. Kiongozi au Mtendaji wa Chama hatakiwi kuwa kiongozi wa Chama chochote cha siasa ingawa anaweza kuwa mwanachama wa Chama chochote cha siasa.

10.11 KURA YA KUTOKUWA NA IMANI

Katika kura ya kutokuwa na imani, ni lazima uamuzi wa kumwondoa kiongozi au uongozi madarakani utokane na theluthi mbili ya idadi ya kura za wajumbe wote wa kikao husika.

10.12 KANUNI MBALIMBALI ZA CHAMA

Chama kitakuwa na kanuni mbalimbali za uendeshaji wa shughuli zake kama ifuatavyo:

1. Kanuni za Uchaguzi;
2. Kanuni za Utumishi;
3. Kanuni za Uongozi;
4. Kanuni za Fedha;
5. Kanuni za Maadili na Utawala Bora;

Kanuni zitaboreshwa kulingana na mahitaji ya kitaalamu ya wakati husika.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

11.0. TAFSIRI

Utata utakaojitokeza kuhusiana na tafsiri ya Katiba hii, utapelekwa kwenye Kamati ya Utendaji ya Taifa kwa ufafanuzi.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI

12.0. KUVUNJIKA KWA CHAMA AU KUUNGANISHA VYAMA

12.1 KUVUNJIKA CHAMA

Chama kinaweza kuacha kufanya shughuli zake na kuvunjwa kama pendekezo litapitishwa na theluthi mbili ya wanachama wote kutoka theluthi mbili ya matawi yote ya chama. Iwapo jambo hili litatokea, mali yote ya chama itakuwa ya Shirikisho husika la Vyama vya Wafanyakazi.

12.2 KUUNGANISHA VYAMA

i. Chama kinaweza kuamua kujivunja baada ya uamuzi wa kutaka kuungana na Chama kingine kufikiwa.
ii. Uamuzi wa kujiunga na Chama kingine unaweza kufikiwa na Mkutano Mkuu wa Chama ukizingatia maoni yaliyowasilishwa kwa njia ya hoja au mapendekezo kutoka katika matawi ya Chama ambayo yanaweza kupigiwa kura na Mkutano Mkuu wa Chama wa Taifa.
iii. Iwapo Chama kitavunjwa na kujiunga na Chama kingine, mali na madeni ya Chama hicho yatachukuliwa na Chama kipya.

SEHEMU YA KUMI NA TATU

13.0. MIGOGORO YA KIKAZI, MIJADALA NA MWENENDO

13.1 SERA YA UJUMLA

Kamati ya Utendaji ya Chama itawajibika katika utekelezaji wa maazimio yanayotokana na majadiliano na migogoro ya Chama lakini itakasimu baadhi ya madaraka yake kwa kamati za kitaalamu na matawi ya chama.

i. Kwa majadiliano yanayohusu sekta nzima ya kikazi, matawi yatashiriki kikamilifu. Katika hali hiyo, Baraza la Majadiliano la Kitaifa linaweza kuanzishwa kwa kuzingatia Kamati za Kisekta ambazo zitafanya majadiliano na Chama cha Waajiri au Mamlaka ya Umma. Wajumbe hawa, kila inapobidi, watashauriana na Katibu Mkuu mtumishi wa Chama.

ii. Matawi yana haki na uhuru wa kujitetea dhidi ya mwajiri na kuendesha shughuli za majadiliano tawini na kupitia Kamati za Kisekta. Matawi yatafanya majadiliano ya kisekta kitaifa.

iii. Ili mgogoro/mgomo ufanikiwe, ni vema kuamua kufanya utaratibu wa kuunga mkono au utaratibu wa vizuizi vya kikazi. Kwa sababu hiyo, ndiyo maana kanuni zinamfanya mwanachama kuheshimu uamuzi uliofanywa na vyombo husika. Hata hivyo, mara nyingi, ni vigumu kuwashawishi wanachama kushiriki katika kuwaunga mkono wanaogoma hasa kama Chama hakiwezi kufidia hasara watakayoipata. Kwa hiyo basi, ili kuweza kupata mapato ya kutosha, itakuwa ni jambo la maana kwa Kamati Kuu ya Uratibu kuanzisha mchango maalum ambao utachangwa na wanachama wasioumia sana kutokana na mgomo.

iv. Mchango maalum unapaswa kutumika, vilevile, kwa ajili ya wanachama walioathiriwa na mgomo wa muda mrefu.

v. Matawi, kupitia Kamati za Kisekta,baada ya kupata ushauri wa kutosha kutoka kwenye chamayatakuwa na uwezo wa kutangaza mgogoro na mwajiri au serikali.